



TANGAZO LA MTIHANI WA USAILI

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) anapenda kuwatangazia waombaji wa nafasi za ajira waliopita mchujo wa awali kwamba mtihani wa usaili wa maandishi (*Aptitude test*) utafanyika Jijini Dodoma, Chuo cha Mipango siku ya tarehe 09.03.2024.

▪ **Mambo muhimu ya Kuzingatia**

1. Tarehe ya usaili ni tarehe 09.3.2024 siku ya Jumamosi;
2. Mtihani utaanza saa 3:00 asubuhi siku hiyo ya tarehe 09.3.2023 kwa waombaji wote;
3. Majina ya waombaji wote walioitwa kwenye usaili pamoja na eneo la kufanya mtihani yanapatikana kwenye wavuti ya TAKUKURU www.pccb.go.tz;
4. Kila mwombaji ajaze taarifa zake binafsi kwenye fomu iliyoambatanishwa na orodha ya majina. Fomu pia inapatikana kwenye wavuti ya TAKUKURU www.pccb.go.tz;
5. Fomu ya taarifa binafsi ijazwe kwa umakini na kwa usahihi. Fomu hiyo ni sehemu ya mtihani wa *Aptitude test*. Mwombaji yejote atakayejaza vibaya Fomu hiyo atakuwa amepoteza nafasi ya kufaulu kwenye usaili huu;
6. Fomu hiyo iwasilishwe siku ya mtihani tarehe 09.3.2024. Msailiwa ambaye hatawasilisha Fomu hiyo atahesabika kuwa ni mionganoni mwa walioshindwa kwenye usaili;
7. Kila msailiwa aandike namba ya mtihani aliyopewa, atakayeandika jina mtihani wake hautasahihishwa;
8. Watakaofaulu kwenye mtihani wa maandishi ndio watakaoitwa kwenye usaili wa mahojiano (*oral interview*).

Imetolewa na;

Mkurugenzi Mkuu,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa,

1 Mtaa wa TAKUKURU S.L.P. 1291,

41101 DODOMA.